BEMBEA YA MAISHA

MFULULIZO WA 2 (DONDOO)

Maswali Matarajiwa ya dondoo Katika Mtihani Mkuu wa KCSE

MFULULIZO WA PILI

Ukihitaji majibu,

Pigia Bw. Isaboke 0746 222 000

AU *0742 999 000*

MWALIMU CONSULTANCY

MARUDIO HALAHALA-MASWALI

1."Maji yangekuwa yamewafika shingo Badi wangeshindwa kuishi Pamoja.Ndoa ni bembea.Kuna wakati itakuwa juu na wakati mwingine chini"

a.weka dondoo hili katika muktadha wake.(al.4)

b)Tambua mbinu za kimtindo katika dondoo hili(al.4)

c)Tambua maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili (al.2)

d)Eleza maudhui uliyotaja hapo juu(al.10)

2."Mungu hakupi yote.Akikupa hiki,anakunyima kile."

a.Weka dondoo hili katika muktadha wake.(al.4)

b.kwa kurejelea tamthilia nzima,fafanua jinsi wahusika wamepewa hiki na kunyimwa kile.(al.16)

(I)kupewa hiki(al.8)

(II)Kunyimwa hiki.(al.8)

3."kukosa Kwa namna yoyote ni umaskini.Mtu Huwa maskini Wa asichokuwa nacho"

a.Weka dondoo hili katika muktadha wake.(al.4)

b.Tambua maudhui katika dondoo hili

c.Fafanua maudhui uliyotambua Kwa kurejelea tamthilia nzima.(al.14)

4."Gongo limeyamega maadili yake kimyakimya na utaratibu Wa uwajibikaji..."

a.weka dondoo hili katika muktadha wake.(al.4)

b.Tambua mbinu za lugha katika dondoo hili.(al.4)

c.Tambua maudhui katika dondoo hili.(al.2)

d.Fafanua athari za maudhui uliyotambua.(al.10)

5."kumbe watoto Hawa tuliowadharau walikuwa nyota ya jaha."

a.weka dondoo hili katika muktadha wake.(al.4)

b.Fafanua jinsi watoto wanaorejelewa walidharauliwa.(al.10)

c.Fafanua namna watoto Hawa wamekuwa nyota ya jaha.(al.6)

6.Baada ya dhiki Faraja.Faraja ni zao LA dhiki.leo kikapu Cha mama kimejaa ndango"

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake (al.4)

b)Taja mbinu mbili za lugha katika dondoo hili (al.4)

c)Taja maudhui mawili yanayojitokeza katika dondoo hili (al.4)

d.kwa kurejelea tamthilia nzima, thibitisha ukweli Wa kauli kuwa 'baada ya dhiki faraja'(al.8)

7."Maisha ya siku hizi SI maji ya kunywa.Yana mashaka tumbi nzima."

a.Eleza muktadha wa dondoo hili.(al.4)

b. Thibitisha kuwa Maisha Yana mashaka tumbi nzima.(al.16)

8.'Alitafunwa kama chingamu lakini naye hakuwa chingamu ya kuisha sukari'(UK.6)

a).Eleza muktadha wa dondoo hili.(Al.4)

b.Bainisha mitindo miwili katika dondoo hili.(al.4)

c)Eleza umuhimu Wa mrejelewa katika kuijenga tamthilia ya 'Bembea ya Maisha(al.12)

9."Mila hizi zinatufanya watumwa"(UK.24)

Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)

b.Fafanua namna Mila zimewafanya watu kuwa watumwa.(al 6)

(c)Eleza umuhimu Wa mzungumziwa katika tamthilia (al.10)

MARUDIO YA BEMBEA YA MAISHA (S2)

10."Mizigo yangu ya majukumu ni mengi"(UK.27)

a.Eleza muktadha wa dondoo hili.(al.4)

b.Thibitisha kauli'mizigo yake ya majukumu ni mingi'kwa kurejelea tamthilia nzima.(al.8)

(c)Eleza umuhimu Wa mzungumzaji Wa maneno haya(al.8)

11.'Ajali Ile ilikuwa mbaya.Majeruhi walihitaji muda Wa kitunzwa'

a.Eleza muktadha wa dondoo hili.(al.4)

(b)Tambua mbinu Moja ya lugha katika dondoo hili.(al.2)

c.Fafanua matumizi ya mbinu uliyotambua hapo juu.(al.14)

12."...mrina haogopi nyuki.."(UK.18)

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili(al.4)

(b) Thibitisha kuwa msemaji Wa kauli hii ana hekima(al.8)

(c)Eleza umuhimu Wa msemewa katika kuijenga tamthilia (al.8)

This Copyright Work belongs to Mwalimu Consultancy 0746222000.

13."Kule shuleni hawafundishi kunga za ndoa.Ndoa ni mtihani mkubwa kabisa"(UK.53)

a)Eleza muktadha wa dondoo hili.(al.4)

b)Tambua sifa nne za mzungumzaji (al.4)

c.Fafanua jinsi ndoa ni mtihani mkubwa(al.12)

14."...Kila limfikalo mwanadamu ni mpango Wa manani.."(UK.12)

(a)Eleza muktadha wa dondoo hili.(al.4)

(b) Thibitisha kauli kwamba 'kila limfikalo mwanadamu ni mpango Wa manani'(al.16)

15."Kazi hizi ni kama safari ya ahera;..."(UK.23)

a.Eleza muktadha wa dondoo hili.(al.4)

b.Tambua maudhui katika dondoo hili.(al.2)

c.Fafanua maudhui uliyotambua Kwa kurejelea tamthilia nzima.(al.14)

16.'Basi tu!Wenzenu ndio walioniingiza katika mkondo huu.kama unakumbuka,nilikuwa miongoni mwa vijana Wa kwanza kuingia Dini.Hata tulikuwa tunahubri,"

a)weka dondoo hili katika muktadha wake (al.4)

b)Eleza madhara ya msemaji kuingia katika mkondo unaorejelewa(al.16)

17."Lakini katika vicheko vyetu zimezikwa kero zetu. Wanavyosema, muungwana hununa moyoni,siyo usoni"

a)weka dondoo hili katika muktadha wake.(al.4)

b)Kwa kurejelea tamthilia nzima,jadili matatizo yanayoikumba jamii.(al.14)

18."Ukilazwa tayari unakuwa meonja seli.Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema.Amri na vitisho kama askari"

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake (al.4)

b)Taja mbinu mbili za kimtindo zilizojitokeza katika dondoo hili.

c)Eleza sifa 4 za msemaji(al.4)

19."Mgala muue na haki umpe"

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake (al.4)

b)Tambua mbinu ya uandishi katika dondoo hili (al.2)

c)Eleza umuhimu Wa mbinu uliyotaja hapo juu (al.2)

d)Kwa kurejelea tamthilia nzima,Eleza jinsi mbinu hiyo imetumika(al.12)

20."Mwanangu,usifanye hofu.Nikujuavyo Mimi,hukuingia katika bahari SI yako.wala hakuna refu lisilokuwa na ncha.Yote Yana kikomo eti.ipo siku haya yote yatapita.Mkulima Hodari ni libasi yake Huwa imechanika na kuchoka lakini moyoni anabaki safi kama theluji Kwa kutosheka na tija ya sulubu zake.Huwezi kumlinganisha na mkulima Wa nguo safi zilizopigwa pasi zikanyooka"

a)Weka dondoo hili katika muktadha wake (al.4)

b)changanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili.

c)Jadili changamoto alizopitia msemaji Wa maneno haya.

21."Maskini mke wangu!Kumbe ugonjwa hukumsaza mwaka baada ya mwaka.umemla bila huruma.Awali niliona kama mchezo.kumbe ilikuwa kweli!kauli yake naona inasimama.Ni mwele hakika.Laiti ningalijua Jana,ningeishi tofauti.Silesi zetu za Maisha tungezila zilivyokuja Kwa furaha."

a)Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)

b)Changanua mtindo katika dondoo hili (al.6)

c)Tambua maudhui matatu katika dondoo hili(al.6)

d)Tambua Toni mbili katika dondoo hili.(al.4)

e)Eleza umuhimu Wa msemaji Wa maneno haya katika kujenga maudhui katika tamthilia.(al.8)

22."kumbuka mrina haogopi nyuki.Marehemu mamangu aliishi kutuambia kuwa nguvu hazimwishi mwanadamu Wala hazipotei bure-humalizwa tu na mabuu.Mwanangu usifanye hofu.Nikujuavyo Mimi, hukuingia katika bahari SI yako"

a)Eleza muktadha wa dondoo hili (al.4)
b)Fafanua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo hili.(al.4)
c)Eleza sifa za msemaji Wa maneno haya (al.12)

23.Haidhuru.umenirudisha nyuma katika siku zile za ujana wangu.Asubuhi Niko skuli majira ya alfajiri.kiboko mkonono,anayekuja baada yangu hata kama hajachelewa Alikuwa Hana lake.siku nzima kazi tu.sio siku hizi,huwezi kumnyoosha mtoto Kwa kiboko.Vitabu navyo nilikuwa navifunga Kwa baiskeli kwenda kuvisahihisha wikendi(UK.62)

a)Fafanua mbinu za kimtindo katika dondoo hili (al.10)
b)Eleza maudhui yanayojitokeza katika dondoo hili (al.10)

24. ***"Mwache mtoto apumzike. Hivi atayashika mangapi?*** **(alama4)**
(a) Eleza muktadha wa dondoo
(b) Eleza umuhimu wa toni ya msemaji wa kauli hii **(alama2)**
(c). Mjadala huu unabainisha majukumu ya watoto kwa wazazi. Thibitisha kwa kuonyesha wazi alivyowajibika anayerejelewa na msemaji katika mjadala.**(alama4)**
(d) Eleza umuhimu wa msemewa katika dondoo hili katika kujenga **tamthilia ya Bembea ya Maisha** **(alama5)**
(e) Eleza sifa tano za mzungumzaji katika dondoo hii **(alama5)**

25. ***Maskini mke wangu! Kumbe ugonjwa haukumsaza mwaka baada ya mwaka. Umemla bila huruma. Awali niliona kama mchezo. Kumbe ilikuwa kweli! Kauli yake ninaona imesimama. Ni mwele hakika. Laiti ningejua, jana ningeishishi tofauti. Silesi zetu za maisha tungezila zilivyokuja kwa furaha. Siku hazigandi wala jana haitarudi. Sasa jana imebaki kuwa kumbukizi baaada ya***

kusombwa na wakati mfano wa mafuriko msimu wa masika. Kwa bahati nzuri bado tupo. Ninaweza kuiachia dunia tabasamu iwe silesi kwa vizazi vijavyo na kila mwenye nia njema. Siwezi kuendelea kuishi hivi. Sasa nimekata shauri. Lazima niache njia ya zamani na kuifuata mpya. Maisha mapya. Pombe! Umenichezesha kama mwanasesere kwa muda mrefu. Umeninyima fursa ya kuilewa familia yangu. Hapana! Siku zangu za uzeeni lazima nizitumie kumwangalia mke wangu mgonjwa. Lazima nimshukuru kwa vitendo kwa jinsi alivyojitolea kuijenga familia yetu. Kwaheri pombe. Buriani.

(a) Changanua mtindo **(alama6)**

(b) Tambua maudhui yoyote matatu yanayojitokeza kwenye kifungu **(alama6)**

(c) Tambua toni mbili inayojitokeza kwenye dondoo hili **(alama4)**

(d) Eleza umuhimu wa msemaji wa maneno haya **(alama4)**

26. *"Mwanangu usifanye hofu. Nikujuavyo mimi, hukuingia katika bahari si yako. Wala hakuna refu lisilokuwa na ncha. Yote yanakikomo eti. Ipo siku haya yote yatapita. Mkulima hodari ni libasi yake huwa imechakaa na kuchoka lakini oyoni anabaki safi kama theluji kwa kutosheka na tija ya sulubu zake. Huwezi kumlinganisha na mkulima wa nguo safi zilizopigwa pasi zikanyooka"*

Chambua mtindo **(alama10)**

Jadili changamoto alizopitia msemewa wa maneno haya **(alama10)**

27. *Mwanangu binadamu mchoyo kwa lake lakini mkarimu ajabu kwa la mwenziwe. Atakukirimu kwa la mwenziwe na atakupa nyongeza usiyohitaji lakini atalizika katika giza kina cha moyo wake. Ndiyo hulka yake hiyo mwana wa Adamu.* '

a) Eleza muktadha wa dondoo hili. **(alama4)**

b) Jadili sifa za msemaji wa maneno haya. **(alama6)**

c) Fafanua umuhimu wa mazungumzo kati ya msemaji na msemewa katika kujenga tamthilia ya Bembea ya Maisha. **(alama10)**

28."***Maisha ya sasa hayana fundi. Yanamwendesha kila mtu kama tawi lilsilosukumwa hadi likang' Oka kutoka tagaani na kupeperushwa na upepo"***

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili **(alama4)**

(b) Tambua vipengele vya kimtindo katika dondoo hili **(alama2)**

(c) Eleza sifa nne za msemewa **(alama4)**

(d) Thibibitisha kauli ya msemaji ukirejelea tamthilia nzima **(alama10)**

29. "***Kumbuka mrina haogopi nyuki. Marehemu mamangu alozoea kutuambia kuwa nguvu hazimwishi mwanadamu wala hazipotei bure; humalizwa tu na mabuu.. usifanye hofu. Nikujuavyo mimi, hukuingia katika bahari si yako. Wala hakuna refu lisilokuwa na ncha. Yote yanakikomo eti. Ipo siku haya yote yatapita. Mkulima hodari ni libasi yake huwa imechakaa na kuchoka lakini moyoni anabaki safi kama theluji kwa kutosheka na tija ya sulubu zake. Huwezi kumlinganisha na mkulima wa nguo safi zilizopigwa pasi zikanyooka"***

(a) Weka dondoo hili katika muktadha wake. **(alama4)**

(b) Tambua mbinu za kimtindo zilizotumika katika dondoo. **(alama4)**

(c) Eleza sifa za msemaji **(alama6)**

(d) Tambua maudhui mawili yanayojitokeza katika kifungu hiki. **(alama2)**

(e) Fafanua maudhui katika swali la (e) kwa kurejelea tamthilia nzima. **(alama4)**

30. "***Ukilazwa tayari unakuwa umeonja seli. Hata wahudumu wenyewe hawana mlahaka mwema. Amri na vitisho kama askari."***

(a) Eleza muktadha wa dondoo hili

(alama4)

(b) Ainisha mbinu mbili za kimtindo katika dondo hili

(alama2)

(c) Eleza sifa nne za msemaji

(alama4)

(d) Dhibitisha kuwa mahali panaporejelewa palikuwa kama seli

(alama4)

(e) Jadili maudhui ya utepetevu kama yanavyojitokeza katika tamthilia nzima **(alama6)**

Ukihitaji majibu,

Pigia bw. Isaboke

THE END

SET BOOKS AVAILABLE WITH US

- ✓ *Artist Of The Floating World*
- ✓ *Bembea Ya Maisha*
- ✓ *Mapambazuko Ya Machweo*
- ✓ *Nguu Za Jadi*
- ✓ *Fathers Of Nations*
- ✓ *Silent Songs And Other Stories*
- ✓ *A Parliament Of Owls*
- ✓ *The Samaritan*

OTHER SETBOOKS GUIDES AVAILABLE				
SETBOOK	**GUIDE**	**QUESTIONS & ANSWERS**	**VIDEOS**	**CONTACT**
Bembea Ya Maisha	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Mapambazuko Ya Machweo	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Nguu Za Jadi	✓	✓	✓	*0746-222-000*
	ENGLISH SETBOOKS			
Fathers Of Nations	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Silent Songs And Other Stories	✓	✓	✓	*0746-222-000*
A Parliament Of Owls	✓	✓	✓	*0746-222-000*
The Samaritan	✓	✓	✓	*0746-222-000*
Artist Of The Floating World	✓	✓	✓	*0746-222-000*

FOR THE FOLLOWING;

- ✓ ONLINE TUITION
- ✓ REVISION NOTES
- ✓ SCHEMES OF WORK
- ✓ SETBOOKS VIDEOS
- ✓ TERMLY EXAMS
- ✓ QUICK REVISION KITS
- ✓ KCSE TOPICALS
- ✓ KCSE PREMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREMOCKS
- ✓ JOINT PREMOCKS
- ✓ KCSE MOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS MOCKS
- ✓ JOINT MOCKS
- ✓ KCSE POSTMOCKS
- ✓ TOP SCHOOLS PREDICTIONS
- ✓ KCSE PREDICTIONS
- ✓ KCSE REVEALED SETS

CALL/TEXT/WHATSAPP

0746 222 000

OR

0742 999 000

mwalimuconsultancy@gmail.com

This is a Product of Mwalimu Consultancy Ltd.

Powered by Mr Isaboke

SUCCESS

REGARDS